REDD net article

Mawasiliano kwa ajili ya Usawa katika Misitu na sera za Tabia nchi

Novemba 2011

# MKUHUMI na Nishati kwa Maendeleo ya Vijijini katika Ukanda wa Afrika Mashariki

Na Richard Kimbowa, David M. Mwayafu na Harriet Smith



Bw. Yusuf Kisiero ambaye hutumia mbinu za kilimo mseto katika Shamba Lake. Kilimo mseto Kumetambuliwa kama majawapo ya kiunganishi kati ya MKUHUMI na kilimo kwa Afrika Mashariki.

## DOKEZO

Waraka huu umechapishwa na mradi wa REDD-net, ambao unafadhiriwa na kitengo cha maendeleo cha Norway (NORAD). Mawazo na mapendekezo yaliyomo kwenye waraka huu ni yale ya waandishi na wala sio ya wafadhili au mashirika yanayoshiriki kwenye mradi wa REDD-net. Utafiti huu ulifanyika kati ya mwezi Juni na Novemba, 2011.

## UTANGULIZI

Neno MKUHUMI linamaanisha Upungazaji wa Hewa Ukaa Kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu ikiwa ni pamoja na shughuli za Uhifadhi, Usimamizi endelevu wa Misitu na Ukuzaji wa Hifadhi za kaboni katika nchi zinazoendelea. Utaratibu huu unalenga kutoa malipo kwa nchi zinazoendelea ili kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa itokanayo na misitu, kwa mfano kupitia kupunguza kushughuli za ubadilishaji wa misitu, usimamizi endelevu wa misitu, na ukuzaji wa vitita vya Kaboni ambavyo vinaweza kujumuisha upandaji wa miti.

## HOJA MUHIMU

Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nishati katika ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na ongezeko la haraka la idadi ya watu ambao wanategemea sana kuni, MKUHUMI inatakiwa kusaidia kupunguza madhara katika rasilimali ya misitu iliyobaki kwa kusaidia upatikanaji wa vyanzo nafuu na mbadala vya nishati.

MKUHUMI inaweza kuchangia zaidi katika malengo ya taifa na kanda katika sekta ya nishati kwa namna zifuatazo:

- MKUHUMI inapaswa kusaidia katika kuboresha usimamizi wa taasisi zinazosimamia misitu pamoja na rasilimali nyingine katika ngazi ya kanda na taifa (Wanasheria katika ngazi ya kitaifa na chini yake).
- MKUHUMI inapaswa kuchangia katika uandaaji wa motisha za kisera pamoja na mipango ya uwekezaji kwa ajili ya kukuza matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati tofauti na mkaa na kuni, na pia kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazosaidia kupunguza matumizi ya nishati katika biashara ndogo na ya kati na pia kwa wakazi wa mjini na vijijini
- MKUHUMI inapaswa kuchangia katika sera na harakati nyinginezo ili kuboresha usanifu katika utengenezaji na utumiaji wa mkaa na kuni katika ngazi zote (kaya, kampuni ya biashara madogo na ya kati).
- Kuna haja ya kuoanisha sera na miundombinu ya kimaendeleo katika sekta ya kilimo, rasilimali za maji, nishati pamoja na sekta nyingine ili kuipatanisha na MKUHUMI na kuzuia migongano.
- Pia, kwa kuongezea kwenye uzoefu uliotokana na mchakato wa R-PP, MKUHUMI inapaswa kusaidia uazishwaji na uimarishaji wa mijadala ili kupata mawazo kwa ajili ya kuzuia migogoro na kuakikisha umiliki wa miradi inayotarajiwa kuhusiana na nishati.

Kuibuka kwa MKUHUMI kunatoa fursa katika ngazi zote za kitaifa na kikanda kuwekeza katika mipango endelevu na ya muda mrefu juu ya uhifadhi endelevu wa misitu. Mipango hii sio tu kwamba inachangia kudhibiti mabidiliko ya tabia nchi kupitia upunguzaji wa ukataji miti na uharibifu wa misitu katika kanda, bali pia inatoa fursa ya kuimarisha mikakati ya kitaifa na kikanda ya kushugulikia maswala ya nishati.

Kwa kuunganisha mikakati ya MKUHUMI na ile ya kitaifa pamoja na mipango mingine ya nishati, itawezekana kufanya yafuatayo:

- kuboresha matumizi endelevu ya nishati itokanayo na mimea pamoja na kutawanyisa vyanzo vya nishati katika maeneo ya mjini na vijijini, na

- kuhifadhi mifumo ikolojia nyeti kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya uzalishaji umeme ambao ni muhimu kwa maendeleo ya viwanda pamoja na huduma za sekta nyingine.

Makala hii imetokana na Makala ya REDD-net juu ya MKUHUMI na sekta nyingine katika Afrika Mashariki (Kimbowa R, et.al, 2011).

## UTANGULIZI JUU YA SEKTA YA NISHATI KATIKA AFRIKA MASHARIKI

Upatikanaji wa nishati umetambuliwa kama mojawapo ya nguzo muhimu katika kufikia dira ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sasa, zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wote waishio katika nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) hawana huduma ya kisasa ya nishati, hali ambayo imefanya nishati za asili kama kuni na mabaki ya mazao yatumike kwa zaidi ya asilimia 80 ya mchanganyiko nishati yote inayoutumika katika kanda (EAC , 2006).

Sehemu kubwa ya nishati ya Majani (biomass) imekuwa ikichomwa katika majiko ya wazi yenye mafiga matatu, hali ambayo uwaweka watumiaji wa majiko hayo katika hali ya hatari kutokana na madhara ya moshi na majanga ya moto. Kupika na kupasha joto ndio matumizi ambayo yanachukua sehemu kubwa ya nishati na pia uchomaji mkaa ni mojawapo ya vichochezi vikuu vya ukataji miti na uharibifu wa misitu katika Afrika Mashariki (GOK, 2010, URT, 2010, GoU, 2011). Shughuli za MKUHUMI zinaweza kuchangia moja kwa moja katika kuhakikisha utawanyishaji wa nishati kupitia ushawishi katika matumizi sanifu ya kuni na pia kupitia msukumo wake katika michakato ambayo itasaidia uratibu katika sekta nyingine (Tazama jedwali Namba 1 kwa ufafanuzi).

Jedwali namba 1:Vyanzo vya Nishati kwa Africa Mashariki

| | Kuni na mkaa | Nishati za kisasa (Umeme, Jua, LPG) |
|---|---|---|
| Kenya | 70% | 30% |
| Tanzania | 90% | 10% |
| Uganda | 93% | 7% |
| EAC | 84% | 16% |

Chanzo: Umoja wa Mataifa, kama ilivyonukuriwa na EAC,2010

## MKUHUMI na Sera za Kikanda na Taifa

Dhana kuu ya Mkakati waJumuiya ya Africa Mashariki juu ya Kukuza Upatikanaji wa Huduma za Kisasa za Nishati, inalenga kuwezesha matumizi ya nishati za kisasa za kupikia miongoni mwa sehemu kubwa ya jamii ambayo bado inatumia teknolojia za zamani katika kupika. Hata hivo, hili kufanikiwa katika lengo hili, inatakiwa kushugulikia pande zote mbili ambazo ni mahitaji (hasa matumizi sanifu ya nishati) na upatikanaji wa nishati (uhifadhi na utunzaji wa nishati)

Malengo na mikakati ya Taifa ya nishati kwa wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki ufuata mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao kwa upande mwingine unaboreshwa na mikakati ya MKUHUMI ambayo imependekezwa kwa lengo la kuhakikisha usalama wa nishati (Jedwali 2 chini). Kutokana na jedwali hili,ni wazi kwamba MKUHUMI na sekta ya nishati zina uhusiano wa karibu sana, hasa kwa upande wa matumizi ya nishati japokuwa hili bado halijaoneka kivitendo hasa kwa vile sera za MKUHUMI ni mpya ambazo zinaanza kutekelezwa Africa Mashariki.

Hata hivyo, pamoja na kwamba sera na mikakati iliyopo inaendana vizuri na MKUHUMI, uchomaji mkaa unabakia kuwa moja ya changamoto kubwa katika nchi zote 3 ambayo inahitaji kutafutiuwa suluhisho kwa mfano (kupitia kuboresha ufanisi, kutunga sheria na sera, na kuendeleza nishati mbadala). Hii nikutokana na utegemezi wa hali ya juu sana wa jamii kwenye mkaa na kuni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 1 (hapo juu).

Kadri sheria, sera na taasisi za kutekeleza MKUHUMI zinavyozidi kuandaliwa, changamoto nazo zimeaza kujitokeza. Kwa mfano, nchini Tanzania, zaidi ya 90% ya nishati yote inayotumiwa utokana na kuni, hali ambayo inaongeza changamoto sana kwenye rasilimali za misitu. Zaidi ya hayo, kumekuwepo na tatizo la ukatikaji umeme wa mara kwa mara katika maeneo ya mijini hata pale ambapo mvua za kutosha zinakuwa zimenyesha na kujaza mabwawa. Hali hii imewalazimu watu kendelea kutegemea sana kuni na mkaa kutokana na upatikanaji wake wa kuaminika. Kwa sababu hiyo, mabadiliko ya nishati kupunguza utegemezi katika kuni na mkaa kama njia ya kupunguza uharibifu wa misitu inaweza kuwa changamoto kubwa sana (URT, 1998)

Kukosekana kwa uratibu na uoanishaji wa sera katika sekta mbalimbali unaweza kukwaza mipango ya MKUHUMI kutokana na kila sekta kujaribu kufanikisha malengo yake binafsi bila kujali sekta nyingine. Kwa mfano, Sera ya Misitu ya Tanzania utambua uhusiano ulipo kati yake na sekta nyingine kama vile kilimo, mifugo, uchimbaji madini, nishati, wanyama pori,ufugaji nyuki, mazingira na ardhi), lakini mapungufu ya kisera katika baadhi ya sekta hizi uchangia kuendelea kwa ukataji miti na uharibifu wa misitu (URT , 1998).

## Jinsi gani MKUHUMI inaweza Kuchangia zaidi katika Malengo ya Sekta ya nishati, katika ngazi ya kitaifana kikanda?

Kutokana na uchambuzi na mjadala hapo juu,yafuatayo ni mapendekezo kwa ajili ya MKUHUMI kuchangia zaidi katika malengo ya sekta ya nishati kwa Afrika ya Mashariki:

- Shughuli za MKUHUMI zinapaswa kusaidia kuboresha usimamizi na utawala katika taasisi husika za misitu na mali asili nyingine katika ngazi ya kanda, taifa na ngazi za chini zaidi (wanasheria katika ngazi ya kitaifa na chini yake). Hii ni kwa sababu watu walio wengi katika ukanda wa Afrika Mashariki wanategemea kuni na mkaa, na kutokana na mahitaji yasiyotabirika ambayo yamezidishwa na upungufu wa umeme, rasilimali za misitu zinakumbana na tishio kubwa la kutoweka (matendo haramu katika uvunaji wa kuni, mbao, na mkaa). Endapo swala hili halitashughulikiwa faida zinazotarajiwa kutokana na MKUHUMI kama vile vitita vya Kaboni, uhifadhi wa vyanzo vya maji, pamoja na huduma nyingine za kimazingira zinaweza kuathirika sana na kwa muda mrefu

- MKUHUMI inatakiwa kuchangia katika sera na hatua nyinginezo kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji mkaa na matumizi ya kuni kuanzia kwa wazalishaji hadi kwa watumiaji ikiwa ni pamoja na makampuni madogo na ya kati).

- MKUHUMI inatakiwa kuchangia katika kuandaa motisha za kisera na mipango ya uwekezaji kwa ajili ya kukuza matumizi ya nishati mbadala dhidi ya mkaa na kuni pamoja na kukuza teknolojia zinazopunguza matumizi ya nishati kwa makampuni ya madogo na ya kati ya biashara, na kwa wakazi wa mijini na vijijini. Mbali na kupunguza shinikizo kwenye rasilimali zilizopo za misitu, jitihada hizi pia zitachangia upatikanaji wa faida kama vile huduma zitokanazo na mifumo ikolojia,

JEDWALI 2: Muhtasari wa Mahusiano kati ya Malengo na Mikakati ya Taifa ya Nishati na Mikakati Iliyopendekezwa MKUHUMI.

| Malengo ya Taifa ya Nishati | Mikakati ya MKUHUMI iliyopendekezwa | Nini zaidi kiongezwe ili kusudi MKUHUMI ichangie zaidi katika kufanikisha malengo ya sekta ya kilimo? |
|---|---|---|
| **Kenya** | | |
| Sheria ya Nishati ya Kenya (2006)<br>• Uendelezaji na Utumiaji wa Teknolojia za Nishati Mbadala (RETs)<br>• Kuwezesha miundombinu ya kisera ili kusaidia ufanisi na uzalishaji endelevu na masoko ya RETs<br>• Kuhimiza matumizi ya miti inayokua haraka kwa ajili ya uzalishaji wa nishati<br>• Kuendeleza teknolojia ya kutengeneza mkaa kwa ufanisi zaidi | • Kuendeleza teknolojia sanifu za uchomaji mkaa<br>• Utekelezaji wa mkakati wa taifa wa maendeleo ya nishati<br>• Kuendeleza mashamba ya miti inayokua haraka kwa ajili ya kuni ufanisi wa nishati<br>• Kuendeleza matumizi ya kijamii ya nishati ya mimea kwa ajili ya kuwashia na kupikia na hivyo kupunguza mahitaji ya kuni.<br>[GOK 2010: pp39 - 40)] | Umakini wa haraka na maalum unahitajika katika kukuza:<br>• Teknolojia sanifu kwa matumizi ya taasisi katika kupika na kukaushia vitu mbalimbali, (kwa mfano mashuleni,makampuni madogo,ya kati na makubwa kama vile yale ya chai, tumbaku na mahospitalini)<br>• Upandaji wa mashamba ya miti inayokua haraka uwe ni jambo la lazima kwa Makampuni makubwa yanayotumia kuni nyingi ili kupunguza madhara yao<br>• Uwepo mgawanyo wa nishati mbadala kulingana na hali halisi katika maeneo husika. Kwa mfano biogesi pale ambapo kinyesi cha ng'ombe na vitu vingine vya namna hiyo vinapatikana, na vile vile nishati ya upepo pale ambapo upepo upo.<br>• Kusimamia uzalishaji na biashara ya kuni na mkaa kwa kutumia mifumo ya jamii ya motisha |
| Mpango wa Mazingira wa Sekta ya Nishati ya Kenya<br>Malengo: Kukuza uzalishaji wa kibiashara ya kuni na kuboresha matumizi sanifu nishati | | |
| Idara ya Nishati mbadala ya Kenya<br>Mikakati: Kukuza uhifadhi wa nishati, ufanisi na vyanzo mbadala vya nishati. | | |

| Malengo ya Taifa ya Nishati | Mikakati ya MKUHUMI iliyopendekezwa | Nini zaidi kiongezwe ili kusudi MKUHUMI ichangie zaidi katika kufanikisha malengo ya sekta ya kilimo? |
|---|---|---|
| **Tanzania** | | |
| Sera ya Taifa ya Nishati, 2003<br>• Kuhakikisha upatikanaji wa vyanzo vya kuaminika na vya gharama nafuu vya nishati pamoja na matumizi yakimanufa na endelevu ya nishati.<br>• Kuanzisha taratibu za ufanisi wa nishati katika uzalishaji, ununuaji, usafirishaji, usambazaji na kwa mtumiaji wa mwisho | • Kuanzisha vyanzo mbadala vya nishati, pamoja na kuongeza ufanisi wa matumizi ya nishati za majani,<br>• Kuendeleza vyanzo mbadala vya nishati dhidi ya kuni.<br>• Usimamizi endelevu wa maeneo nyeti ya maji kwa ajili kulinda utililikaji thabiti wa maji kwa ajili ya kuzalisha umeme wa mabwawa<br>[URT 2010: pp83] | • Kuongeza matumizi bora ya nishati ya majani kwa kukuza teknolojia na matendo bora ya kupika na kukausha katika taasisi (kwa mfano mashuleni, makampuni  madogo,ya kati na makubwa ya biashara yanayotumia kuni nyingi kama yale ya chai, tumbaku na mahospitalini)<br>• Umakini maalum na wa haraka katika kukuza teknolojia na ufanisi katika kutengeneza makaa<br>• Kusimamia uzalishaji na uuzaji wa kuni na mkaa kwa kutumia mifumo ya jamii ya motisha |
| **Uganda** | | |
| Sera ya Nishati Mbadala (2007)<br>Lengo kuu la Sera: kukuza matumizi ya nishati mbadala ya kisasa, kutoka asilimia 4% za sasa hadi asilimia 61% za matumizi yote ya nishati kwa mwaka 2017<br>Mikakati<br>• Kudumisha na kuboresha mwitikio wa mifumo ya kisheria na kitaasisi katika kuwezesha uwekezaji katika nishati mbadala<br>• Kuanzisha utaratibu maalum wa kifedha na sera ili kuvutia uwekezaji zaidi na pia kuwezesha RETs kupenya masoko mengi zaidi.<br>• Kukuza mifumo ambayo uongeza uwezo wa watoa huduma wa umma na binafsi katika masuala ya nishati keudeleza na kukuza teknolojia amabazo zinazingatia maswala ya jinsia karika teknolojia za nishati mbadala<br>• Kukuza mifumo ya ushirikiano wa kimataifa katika utafiti na maendeleo,<br>• Ubadilishanaji wa teknolojia pamoja na viwango sahihi husika.<br>• Kusimamia rasilimali za nishati majani kwa njia endelevu<br>• Hamasisha matumizi ya nishati hai katika nchi na hasa katika sekta ya usafiri,<br>• Kukuza ubadilishaji wa taka za manisipaa na viwandani kuwa nishati | Uchaguzi wa Kimkakati: Kushughulikia athari zitokanazo na uzalishaji na utumiaji wa mkaa usio endelevu.<br>• Kudhibiti uzalishaji na biashara ya mkaa<br>• ufafanuzi wa maswala ya umiliki wa ardhi na mti kwenye mashamba binafsi<br>• Kuboresha ufanisi wa matumizi ya mkaa<br>• Kuimarisha usimamizi na utiifu<br>• Kufanya mageuzi ya sera katika Sekta ya Nishati ili kuwezesha ukuaji (kupitia motisha) na maendeleo ya vyanzo mbadala na nafuu  vya nishati ili kupunguza shinikizo juu ya nishati ya majani<br>• Uchaguzi wa Kimkakati: Kushuguria athari za uvunaji na utumiaji kuni kutoka katika rasilimali za mistitu nchini Uganda.<br>• Kuongeza majani / miti katika mashamba<br>• Kukuza matumizi sanifu ya kuni<br>• Kuendeleza vyanzo mbadala na nafuu vya nishati safi kwa watumiaji wakubwa wa kuni<br>• Kuanzisha vitalu vya kupandia, ili kukuza usimamizi endelevu na uzalishaji wa rasilimali za misitu pamoja na kuunda utarati wa kusimamia viwanda vya usindikaji wa mbao (matumizi sanifu ya miti kwa ajili ya mbao na bidhaa nyinginezo za mbao).<br>[Gou, 2011: pp87-90] | Umakini wa haraka na maalum katika kukuza:<br>• Usanifu wa taasisi katika teknolojia za kupika na kukausha (kwa mfano mashuleni, makampuni madogo, ya kati na makubwa  ambayo yanatumia kuni nyngi kama yale ya chai, tumbaku na mahospitali,)<br>• Upandaji wa mashamba ya miti inayokua haraka uwe ni jambo la lazima kwa Makampuni makubwa yanayotumia kuni nyingi ili kupunguza madhara yao<br>• Uwepo mgawanyo wa nishati mbadala kulingana na hali halisi katika maeneo husika.  Kwa mfano biogesi pale ambapo kinyesi cha ng'ombe na vitu vingine vya namna hiyo vinapatika, na vile vile nishati ya upepo pale ambapo upepo upo.<br>• kusimamia uzalishaji na biashara ya kuni na mkaa kwa kutumia mifumo ya jamii ya motisha |

uhifadhi wa vyanzo vya maji pamoja na uhifadhi ya bioanuai.

- Kuna haja ya kuoanisha sera na sheria nyingine za kilimo, rasilimali za maji, nishati na sekta nyinginezo ili kuendana na MKUHUMI ili kuzuia kukinzana kwa mipango. Kwa mujibu wa ukuaji tarajiwa katika uchumi na idadi ya watu, utenganishaji wa nishati na sekta nyingine kunaweza kusababisha migongano zaidi ya kimadaraka na kuathiri sana uendelevu wa ardhi, maji, bioanuai na rasilimali nyinginezo.

- Pia, kwa kuongezea kwenye uzoefu uliotokana na mchakato wa R-PP, MKUHUMI inapaswa kusaidia uazishwaji na uimarishaji wa mijadala ili kupata mawazo na maoni kwa ajili ya kuzuia migogoro na kuakikisha

umiliki wa ardhi kwa jamii husika hasa katika maendeleo yanayotokana na shughuli za nishati.Hii inaweza kujumuisha mikutano ya mara kwa mara, majadiliano na marejesho juu ya mipango inayotarajiwa kutekelezwa, uandaaji wa sera, na pia mapitio na maboresho katika sera nyeti kama vile upandaji wa bei za umeme, ushuru katika biashara ya mkaa na kuni, uhamisho wa watu n.k. Yote haya yanaweza kuwasaidia wadau kuchangia katika kuandaa mfumo endelevu wa nishati.

## MAREJELEO YALIYOTAJWA PAMOJA NA VYANZO ZAIDI VYA TAARIFA


ERA (2010) Ushuru Nishati Mbadala nchini Uganda (REFIT).Awamu ya Pili, Miongozo iliyopitishwa kwa kipindi cha 2011-2012, Tovuti, http://www.era.or.ug/pdf/Approved_Uganda%20REFIT%20Guidelines%20V4%20%282%29.pdf. Imetembelewa Septemba 2011

EAC (2006).Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki 2006-2010. Kukuza na kuendeleza muungano.

EAC (2010). Repoti ya ukweli na takwimu,Tovuti:http://www.eac.int/statistics/index.php?option=com_docman&task=doc_view&gid=131&tmpl=component&format=raw&Itemid=153, imetembelewa Julai 4, 2011

EAC(2009). Mkakati wa kikanda juu ya Ukuzaji wa Upatikanaji wa huduma za nishati ya kisasa katika Afrika Mashariki

GoK (2006). Sheria ya Nishati: http://www.erc.go.ke/energy.pdf, imetembelewa Septemba 2011

GoK (2010). Mapendekezo yaliyoboreshwa juu ya Utiyari wa MKUHUMI kwa Kenya. www.forestcarbonpartnership.org/fcp/sites/forestcarbonpartnership.org/files/Documents/PDF/Oct2010/Revised 20RPP% 20for%% 20Kenya.pdf, Tovuti hii ilitembelewa Juni 20

GoU (2001).Sera ya Taifa ya Misitu. Wizara ya Maji, Ardhi, na Mazingira

GoU (2002).Sera ya Nishati ya Uganda. Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini

GoU (2007).Sera ya Nishati Mbadala ya Uganda. Wizara ya Nishati na Maendeleo ya Madini:http://www.rea.or.ug/userfiles/RENEWABLE%20ENERGY%20POLIC9-11-07, Imetembelewa Septemba 2011

GoU (2011)Mapendekezo yaliyoboreshwa juu ya Utiyari wa MKUHUMI kwa Uganda ambayo yalikabidhiwa kwa mfuko wa Benki ya Dunia wa Ushirika wa Kaboni ya Misitu. http://www.forestcarbonpartnership.org/fcp/sites/forestcarbonpartnership.org/files/Documents/PDF/June2011/Uganda%20/Revised 20RPP% 20May 2031%2C%20%20 2011_O.pdf ,Kenya.pdf, Tovuti hii ilitembelewa Juni 2011

Mpango wa Mazingira wa Sekta ya Nishati wa Kenya (2011): http://www.kengen.co.ke/index.php?page=business&subpage=ke, imetembelewa August 4 2011

Kimbowa R, Mwayafu M.D.,& Kairu G. (2011). Makala ya Uchambuzi: MKUHUMI na Sekta nyingine katika Afrika Mashariki. Chapisho la REDD-net

URT (1998) Sera ya Taifa ya Misitu Tanzania. 1998 Dar es Salaam

URT (2003) Sera ya Taifa ya Nishati. Wizara ya Madini na Nishati: http//tatedo.org/cms/images//publications/reports/energypolicy.pdf, Imetembelewa Septemba 2011

URT (2010) Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa Kutokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI/REDD+): Mpango wa MKUHUMI Tanzania: http://www.reddtz.org/content/view/22/26, Imetembelewa Juni 2011


## KUHUSU REDD-NET

REDD-net ni jukwaa la maarifa la kimataifa kwa mashirika ya kiraia kusini mwa dunia ambalo huyawezesha kupata habari kuhusu juhudi za Upunguzaji wa Uzalishaji wa hewa ya ukaa kutokana na Ukataji na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI+), na pia kupata fursa ya kubadilishana uzoefu wao wenyewe na kusaidiana kuandaa miradi na sera za kutekeleza miradi ya MKUHUMI+ ambayo inawelenga zaidi maskini.
Jukwaa hili la REDD-net ni ushirikiano kati ya mashirika ya Centro Agrononómico Tropical de Investigación y Enseóanza (CATIE), Overseas Development Institute (ODI), RECOFTC - The Center for People and Forest na Uganda Coalition for Sustainable Development (UCSD). REDD-net inafadhiliwa serikali ya Norway yaani 'Norad'.

Kwa habari zaidi kuhusu mradi huu wasiliana Kristy Graham wa ODI kupitia barua pepe (k.graham @ odi.org.uk). Kwa habari zaidi juu ya REDD-net Afrika Mashariki tafadhali wasiliana na David Mwayafu wa UCSD kupitia barua pepe (dmwayafu@ugandacoalition.or.ug).

KWA TAARIFA ZAIDI KUHUSU REDD-NET TEMBELEA : WWW.REDD-NET.ORG